KUFICHUA MADAI YA UWONGO

COVID-19 NA JAMII ZA WAHAMIAJI NA WAKIMBIZI

Kama watu wanaopenda kujumuika pamoja, tunategemeana ili kuishi. COVID-19 imetupa changamoto sisi sote kuuliza swali, “tunaweza kutegemeana vipi bila kuhatarisha usalama wetu na usalama wa wapendwa wetu?”. Tunapenda familia zetu, lakini tungependa sisi sote tuendelee kuishi. TUNAHITAJI kuishi. Njia pekee ya kuhakikisha hili linafanyika ni kuzuia kuenea kwa COVID-19. Tunapokaribia kufikia mwaka mmoja tangu COVID-19 ianze, tungependa kuwakumbuka na kuwaheshimu wanajamii ambao tumepoteza wakati huo huo tukitambua dhana potofu kuhusu COVID-19 ili tuweze kupambana na hali hii na kuwa wenye afya na salama.

UWONGO: Hali za ustawi wa jamii na uhamiaji zinahitajika ili kupimwa COVID-19.

UKWELI: Kuenda kupimwa hakuhusiani na uhamiaji; hawatakuuliza swali lolote linalohusu hayo. Wahamiaji ambao hawajasajiliwa rasmi nchini wanaweza kupimwa, na maafisa wa afya hawatauliza kuhusu hali yao ya uhamiaji.[1]



Afya ya Umma ya Denver inatoa upimaji wa bila malipo kwa COVID-19 katika maeneo mbalimbali ya jamii katika Denver. Upimaji hutolewa kwa mtu yeyote licha ya kuwa na au kukosa bima au hali yake ya uhamiaji, na hakuna miadi au usajili wa mapema unaohitajika.

UWONGO: Ikiwa nitapimwa hospitalini au kliniki, ninaweza kupata COVID-19 huko.

UKWELI: Mwanzoni mwa janga hili, huenda ulikuwa na wasiwasi kuwa kwenda kumuona daktari kutakuweka katika hatari ya kuambukizwa. Hospitali ni salama kuliko duka la vyakula au mkahawa wako wa kawaida. Kuna hatua kali za kiusalama zinazochukuliwa katika hospitali na kliniki.[2] Wafanyakazi wa huduma ya afya huzingatia hatua za juu zaidi za kiusalama; huenda uko salama zaidi ukiwa huko.

1 Moreno, Graciela. “Latino Life: Walatini Zaidi katika California Wanafariki Kutokana na COVID-19.” ABC30 Fresno, KFSN-TV, 23 Agosti 2020, abc30.com/latino-life-coronavirus-latinos-latinos-fresno/6384623/.

2 Cabotaje, Angela. “Ufichuzi wa Madai ya Uwongo kuhusu COVID-19.” Right as Rain na UW Medicine, 19 Oct. 2020, rightasrain.uwmedicine.org/well/health/covid-myths-debunked.

TAJA MAHITAJI YAKO

JINSI YA KUJITETEA WEWE MWENYEWE KWA WAKATI HUU!

Rashid Ullah alizaliwa Burma. Rashid aliishi katika kambi ya Wakimbizi ya Bangladeshi kwa karibu miaka 16 na alifika Marekani mnamo 2009. Tangu mwaka wa 2015, Rashid amefanya kazi ya kujitolea kwa Jumuiya ya Kiislamu ya Burma katika Colorado.

MASWALI NA MAJIBU!

Rashid Ullah
MSHIRIKA WA JAMII

SWALI:
Je, ni dhana gani potofu zaidi ambayo umewahi kusikia katika jamii yako kuhusiana na COVID-19?

JIBU:
Watu wanafikiria kuwa kutumia vifaa vya kinga binafsi na kudumisha umbali wa kijamii kunaweza kupunguza kabisa uwezekano wa kupata virusi lakini bado watu wanapata COVID-19.

SWALI:
Je, watu katika jamii yako wanawezaje kupata uwezeshaji wakati huu?

JIBU:
Kutafuta rasilimali kwa kila mmoja na kuendelea kushirikiana kama jamii. Katika nyakati hizi tunapaswa kutegemeana.

SWALI:
Je, ni rasilimali gani za jamii zinazoaminika za COVID-19 kila mtu anapaswa kuzingatia?

JIBU:

- **Kufuata miongozo ya idara ya afya**
- **Kuendelea kufahamishwa na CDPHE na CDC**

USHAURI KUTOKA KWA ADRIEN MATADI

Adrien Matadi alizaliwa Kinshasa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, wakati huo ilijulikana kama Zaire. Adrien alifika Marekani mnamo 2006 na anafanya kazi kama Msaidizi wa Mawasiliano ya Huduma katika Kliniki ya Wakimbizi ya Denver Health. Amefanya kazi kama afisa wa ushirikiano wa jamii na mfanyakazi wa jamii kwa wakimbizi na wahamiaji wa Kiafrika katika Shirika la Colorado la Kiafrika. Adrien anajua lugha kadhaa, ikiwa ni pamoja na Kifaransa, Kiarabu, Kiamhariki na Kiswahili.

Adrien Matadi
AFISA WA USHIRIKINO WA JAMII NA MFANYAKAZI WA JAMII KWA WAKIMBIZI NA WAHAMIAJI WA KIAFRIKA

"Watu katika jamii zetu wanaweza kupata uwezeshaji katika wakati huu kwa aidha kuandaa au kuhudhuria mikutano ya mtandaoni ya ukumbi wa mji kuhusu COVID-19. Ni muhimu kuwa na maelezo sahihi kuhusu COVID-19 na chanjo. Maelezo muhimu zaidi ninayo kwa jamii zinazojaribu kukabiliana na COVID ni kusikiliza taarifa kutoka kwa vyanzo na maafisa wa kuaminika. Wazee, viongozi wa jamii na viongozi wa kidini wanaweza pia kutumiwa kama rasilimali zinazoaminika za jamii kuhusiana na COVID-19."

Mojawapo ya dhana potofu zaidi ni kwamba wakazi wengi wa miji wanaweza kupata taarifa za kidijitali kuhusu janga. Wanajamii wanaweza kupata uwezeshaji wakati huu ikiwa kuna maelezo kuhusu COVID-19 katika lugha nyingi.

Jinsi ya kulipia misaada ya COVID-19?

- **Katika Colorado, Medicaid ya Dharura itashughulikia gharama za kwenda kwenye chumba cha dharura na kulazwa hospitalini kutokana na COVID-19. Mara tu utakapoondoka hospitalini, Medicaid ya dharura itagharamia oksijeni na ziara mbili za huduma za msingi. 3**
- **Medicaid ya dharura inapatikana kwa wasio na bima na au watu ambao hawajasajiliwa rasmi nchini.**
- **Gharama ya kusaidia watu wasio na bima haihamishiwi kwa umma.**
- **Denver Health ni mahali salama kwa wagonjwa. Habari ZOTE zinazohusu mgonjwa zinawekwa salama. https://www.denverhealth.org/patients-visitors/amenities-experience/immigrant-refugee-patient-rights**

Mwongozo wa Nyenzo!

- **Pata Kituo cha Rasilimali za Virusi vya Korona kwa Jamii ya Wahamiaji katikawww.UnitedWeDream.org.**
- **Pata Ustahiki wa Wahamiaji kwa Mipango ya Umma Wakati wa COVID-19 katikawww.ProtectingImmigrantFamilies.org.**
- **Aunt Bertha Social Care Network Pata msaada wa chakula, usaidizi katika kulipia bili, na mipango ya bila malipo au iliyopunguzwa bei, ikiwa ni pamoja na mipango mipya kuhusiana janga la COVID-19 katika findhelp.org**
- **Pata Mwongozo wa COVID-19 wa Maabara za Usawa unaopatikana katika www.EqualityLabs.org/covid19guide katika lugha nyingi: Kiingereza, Kihindi, Kitamil, Kitelugu, Kigujarati, Kimalayalamu, Kikannada, Kipunjabi, Kiurdu, Kinepali, Kiburma, Kibengali na Kimarathi.**

"Haki za Wakimbizi na Wahamiaji Wagonjwa." Haki za Wakimbizi na Wahamiaji Wagonjwa | Denver Health, 2020, www.denverhealth.org/patients-visitors/amenities-experience/immigrant-refugee-patient-rights.